



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA

MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA



ISO 9001: 2015 IMETHIBITISHWA

TAARIFA KWA UMMA

UWEPO KATIKA SOKO WA SIGARA AINA YA *BHARATH SPECIAL BEEDIES* AMBAYO HAIJATAMBULIWA WALA KUSAJILIWA NA TMDA

1. Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), kwa mujibu wa Sheria ya Udhhibiti wa Tumbaku, Sura 121, ilimepewa jukumu la kudhibiti bidhaa za tumbaku katika soko kupitia Tangazo la Serikali (Tobacco Products (Regulations) (Designation of Inspectors) Notice, 2021).
2. Katika utekelezaji wa jukumu hilo na kwa kupitia mifumo ya ukaguzi na ufuatiliaji wa bidhaa za tumbaku katika soko, TMDA inapenda kuutangazia umma kwamba imebaini uwepo wa sigara zenye jina la *Bharath Special Beedies* ambazo hazijatambuliwa wala kusajiliwa na Mamlaka. Kwa mujibu wa maelezo katika lebo, sigara hizo zinatengenezwa na kiwanda cha *Bharath Beedi Works Private Limited, P.B No. 730, Mangalore - 3 PH: 0824 – 2443030, India*.
3. Ukaguzi na ufuatiliaji uliofanywa na TMDA na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kwa kushirikiana na vyombo vya usalama umebaini kuwa sigara hizo ambazo zipo katika muundo wa msokoto huingizwa nchini kinyume cha sheria na kuuzwa kwa kificho katika vibanda na maduka ya biashara mchanganyiko (jumla na rejareja) yenye mikusanyiko ya watu hususan mijini katika mikoa ya Mwanza, Geita, Kigoma, Tabora, Songwe na Mbeya.

4. Aidha, katika kufanya biashara hiyo kwa kificho, sigara hizo huuzwa kwa siri kwa kutumia majina yasiyo halisi kama vile sigara mnato, sigara kali au shkata.
5. Muonekano wa vifungashio vya nje na ndani kama unavyoonesha katika picha Na.1 na 2 hapa chini.

Picha Na. 1: Kifungashio cha nje



Picha Na. 2: Vifungashio vya ndani



6. Hivyo, kutokana na kubainika kwa sigara hizi katika soko kinyume cha sheria, TMDA inawaelekeza wale wote wanaojihusisha na uvutaji wa sigara hizi kutozitumia kwa sababu hazijatambuliwa wala kusajiliwa na Mamlaka. Aidha, uchunguzi zaidi wa kimaabara unaendelea ili kubaini viambato halisi vilivyopo katika sigara hizi. Aidha, wafanyabiashara wanaelekezwa kutojihusisha na biashara ya sigara hizi kwani hatua za kisheria tayari zimeanza kuchukuliwa dhidi ya waliokamatwa wakitunza na kuuza sigara husika.
7. TMDA inawaomba pia wananchi kuendelea kutoa taarifa katika ofisi za TMDA na katika vyombo vya usalama vilivyo karibu endapo watabaini mtu, kampuni au kikundi chochote kinachojihusisha uingizaji, usambazaji au uuzaji wa bidhaa hii ya tumbaku ili hatua za kisheria ziweze zichukuliwe.


Imetolewa na:

**Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA),
Jengo la PSSF, Ghorofa ya 10, Barabara ya Makole,
S. L. P 1253, Dodoma au
S. L. P 77150, Dar es Salaam
Simu: +255 22 2452108/2450512/2450751
Nukushi: +255 22 2450793
Simu bila malipo: 0800110084**